

**SWALI:** Nini maana ya Zaburi 125:3 “ Kwa maana fimbo ya udhalimu  
Haitakaa juu ya fungu la wenye haki; Wenye haki wasije wakainyosha  
Mikono yao kwenye upotovu”.

---

**JIBU:** Mstari huo unatuonyesha jinsi Mungu anavyowatenga watu wake  
na adhabu ambazo zinawahusu waovu. Kwamba kamwe fimbo ya  
adhabu haiwezi kuwahusu watu wa Mungu, Ndio maana ya hilo neno  
‘Kwa maana fimbo ya udhalimu Haitakaa juu ya fungu la wenye haki;..  
Ni mfano tu wa wana wa Israeli wakati ule walipokuwa Misri, Mungu  
aliwatenga na wamisri na kuwaweka kule Gosheni, na mpigo yote  
yalipokuja hayakuwakuta wana wa Israeli, bali wamisri tu. Hata  
baadaye alipotaka kuliadhibu taifa zima, bado aliwaficha watu wake  
ndani ya nyumba, na Yule malaika aliyeshushwa kuwauwa watu,  
hakupita katika nyumba zao. Kuonyesha kuwa fimbo za makosa Mungu  
hana desturi ya kuzijumuisha na watu wake, isipokuwa tu wamekataa  
wenyewe. Ndivyo ilivyokuwa kwa Nuhu, na Lutu.

Na anafanya hivyo kwasababu gani? Ndio hapo anasema ili “Wenye haki  
wasije wakainyosha Mikono yao kwenye upotovu”. Kwamba  
anawataadharisha watu wake wasidiriki kufanya makosa kama hayo  
hayo ya waovu kwasababu na wenyewe adhabu inaweza kuwakuta

Fahamu maana ya Zaburi 125:3 “ Kwa maana fimbo ya udhalimu  
Haitakaa juu ya fungu la wenye haki.

vilevile. Na kweli ndivyo ilivyokuwa kwa wana wa Israeli baadaye,  
walimwacha Mungu wakaanza kuitumikia miungu, na matokeo yake  
Mungu akawarudisha tena utumwani, na miji yao kubomolewa.

Hivyo, ni kutuonya kuwa sisi tuliokoka, kamwe tusijichanganye na  
maovu kwasababu adhabu ya makosa yaweza kutupata na sisi pia,  
kwasababu Mungu hatazami uso wa mwanadamu, bali ulekevu wako  
kwake.

Shalom.

Kwa maana nyingine ya mistari mbalimbali ya biblia tembelea website  
yetu hii >>> [www.wingulamashahidi.org](http://www.wingulamashahidi.org).

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

**Mada Nyinginezo:**

Fahamu maana ya Zaburi 125:3 “ Kwa maana fimbo ya udhalimu  
Haitakaa juu ya fungu la wenye haki.

**Kulabu ni nini katika biblia?(2Wafalme 19:27)**

**Miimo ni nini na kizingiti ni nini?**

**Tirshatha ni nini? (Ezra 2:63)**

**Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma.**

**TUNAHESABIWA HAKI BURE KWA NJIA YA IMANI.**

**Je Bwana Yesu aliruhusu wanafunzi wake kubeba Fimbo au  
hakuwaruhusu? (Marko 6:8 na Mathayo 10:10).**

**Tofauti kati ya zaka na sadaka ni ipi?**

**UTARATIBU WA KUTOA FUNGU LA 10 UPOJE?.**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp

Print this post